**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# MWONGOZO WA URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YAKISERIKALI TANZANIA BARA

**TOLEO LA TATU: AGOSTI, 2025**

YALIYOMO


**DIBAJI** ....4

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ....1

**Usuli** ....1

**Tafsiri ya Shirika Lisilo la Kiserikali** ....3

**Malengo ya Mwongozo** ....3

**Walengwa wa Mwongozo** ....5

**Muundo wa Mwongozo** ....5

**SURA YA PILI: MFUMO WA KISHERIA** ....6

**Utangulizi** ....6

**Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023** ....6

**Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia Kanuni Na. 609 ya mwaka 2018** ....8

**Mafanikio Yaliyopatikana Kutokana na Mabadiliko Yaliyofanyika Kupitia Kanuni Na. 609 ya mwaka 2018 na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.** ....9

**Changamoto** ....10

(i) **Muingiliano na Mgongano wa Kiutendaji na Kiuratibu** ....10

(ii) **Utegemezi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa Wafadhili** ....11

(iii) **Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Mengi Kujikita Maeneo ya Mijini** ....11

(iv) **Ukosefu wa Misingi ya Uwazi na Uwajibikaji** ....11

(v) **Kutotumika kwa Utaalam katika Utekelezaji wa Afua** ....11

**Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto** ....12

**SURA YA TATU: MAJUKUMU YA WIZARA, IDARA NA TAASISI ZA SERIKALI, SEKRETARIETI ZA MIKOA, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA, BARAZA LA TAIFA LA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NaCoNGO), SEKTA BINAFSI NA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI** ....13

**Utangulizi** ....13

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum** ....14

**Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa** ....16

**Majukumu ya Afisa Dawati katika Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa** ..17

**Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu(FIU) kilicho chini ya Wizara hiyo kitakuwa na majukumu yafuatayo:** ....19

**Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi** ....20

**Wizara za Kisekta** ....22

**Idara na Taasisi za Serikali** ....23

**Idara na Taasisi za Serikali zitakuwa na majukumu yafuatayo,** ....23

Wakuu wa Mikoa na Sekretarieti za Mikoa ........ 25
Wakuu wa Mikoa ........ 25
Makatibu Tawala wa Mikoa ........ 25
Wasajili Wasaidizi katika Mikoa ........ 26
Wakuu wa Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa ........ 27
Makatibu Tawala wa Wilaya ........ 28
Wasajili Wasaidizi katika Halmashauri ........ 29
Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) ........ 30
Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 31
(i) Mashirika ya Kitaifa ........ 31
Sekta Binafsi ........ 36
SURA YA NNE: MIKUTANO YA MAJADILIANO NA JAMII PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MILA NA DESTURI ZA KITANZANIA ........ 38
SURA YA TANO: UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MWONGOZO ........ 39
SURA YA SITA: HITIMISHO ........ 41
VIAMBATANISHO ........ 42

## DIBAJI

Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka (2001) inaweka msingi wa uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini na kuweka mazingira wezeshi ya utendaji kazi wa Mashirika hayo kwa kutoa maana ya Shirika Lisilo la Kiserikali, kuainisha vyombo vya usimamizi vya Mashirika na kuweka utaratibu wa kusajili Mashirika. Sera hii ndiyo msingi wa kutungwa kwa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023.

Mwongozo huu utasaidia kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kuimarisha uwazi na uwajibikaji na kuimarisha ushirikiano katika utendaji na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali baina ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika yenyewe katika kufanya shughuli za maendeleo.

Utekelezaji wa Mwongozo huu utaenda pamoja na utekelezaji wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023 na Kanuni zake, katika kusimamia utendaji na ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pamoja na kutatua changamoto mbalimbali zilizopo katika Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Serikali inaamini kuwa mwongozo huu utaimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yaweze kutoa mchango wao kikamilifu katika maendeleo ya nchi.

Dkt. John A.K. Jingu
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## Usuli

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ajili ya kuweka misingi imara ya ushirikiano wa pamoja na kuainisha majukumu kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kusimamia na kuratibu utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini.

Msingi wa Mwongozo huu ni kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001. Sera inaelekeza kuweka mifumo thabiti ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi zote ili kuwezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushiriki ipasavyo katika ajenda ya maendeleo ya Taifa. Aidha, Mwongozo utarahisisha utekelezaji wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023 pamoja na Kanuni zinazosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Sheria nyingine za Nchi.

Mwongozo huu pia umetokana na upungufu katika masuala ya uwazi na uwajibikaji kwa baadhi ya Mashirika hasa katika mapato na matumizi ya fedha na hivyo Serikali kushindwa kutambua michango ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika pato la Taifa na maendeleo ya jamii. Aidha, imejitokeza hali ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza miradi na afua mbalimbali zinazofanana katika eneo moja na kwa walengwa wa aina moja, na hivyo kusababisha maeneo mengine kutofikiwa na huduma zitolewazo na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Mwongozo huu utasaidia kuondoa mgongano wa kiutendaji na kuimarisha uratibu wa pamoja wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika

kuhakikisha kuwa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini inaratibiwa vyema na kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kudhibiti vitendo vilivyo kinyume na Sheria, Kanuni na maadili ya nchi.

**Tafsiri ya Shirika Lisilo la Kiserikali**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023, Shirika Lisilo la Kiserikali ni kikundi binafsi na cha hiari cha watu au mashirika, kisicho cha kisiasa wala kidini, kisicho cha kugawana faida, ambacho kimeundwa katika ngazi ya jamii kitaifa na kimataifa, chenye dhamira ya kukuza malengo halali ya kiuchumi, kijamii au kiutamaduni, kuhifadhi mazingira, kulinda na kutetea hakiza binadamu na utawala bora katika jamii.

**Malengo ya Mwongozo**

Lengo kuu la Mwongozo ni kuondoa muingiliano na mgongano wa kiutendaji na kuimarisha uratibu wa pamoja wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Malengo Mahsusi ni:

(i) Kutoa uelewa kuhusu tafsiri ya Shirika Lisilo la Kiserikali iliyotolewa chini ya marekebisho ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023;

(ii) Kuainisha majukumu ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), na Sekta Binafsi katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(iii) Kuhimiza umuhimu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia dhana ya uwazi na uwajibikaji;

(iv) Kuhimiza umuhimu wa kutekeleza miradi ambayo ina matokeo chanya kwa maendeleo ya walengwa na jamii; na

(v) Kuweka utaratibu wa kufanya mawasiliano ya mara kwa mara na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhusiana na shughuli zote za utekelezaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zinazoendelea katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

**Walengwa wa Mwongozo**

Mwongozo huu unalenga kutumiwa na Wizara yenye dhamana na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

**Muundo wa Mwongozo**

Mwongozo huu unajumuisha Sura kuu tano ; Sura ya Kwanza inatoa maelezo yaUtangulizi, Tafsiri ya Shirika Lisilo la Kiserikali, Malengo na Walengwa wa Mwongozo. Sura ya Pili inaelezea mfumo wa Kisheria ikihusisha marekebisho ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Kanuni zake; mafanikio yaliyopatikana kutokana na mabadiliko yaliyofanyika kupitia Kanuni Na. 609 ya mwaka 2018; Changamoto; na Mikakati ya kukabiliana na changamoto. Sura ya Tatu inabainisha Majukumu mbalimbali ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Sura ya nne inaelezea Mikutano ya majadiliano na jamii pamoja na uzingatiaji wa mila na desturi za kitanzania, Sura ya tano inaelezea Ufuatiliaji na Tathmini ya Mwongozo.

## SURA YA PILI: MFUMO WA KISHERIA

### Utangulizi

Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 ilipelekea kutungwa kwa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023. Lengo kuu ni kuweka misingi imara ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa Sera na Sheria.

### Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023

Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023 pamoja na mambo mengine: -

(i) Inatoa tafsiri ya Shirika Lisilo la Kiserikali kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu cha 3 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023;

(ii) Kifungu cha 32(1) cha Sheria hii, kinayataka Mashirika yote yaliyosajiliwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa nyaraka zao za usajili yaani Katiba na cheti cha usajili;

(iii) Kuainisha vyombo vya kisheria vya usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwemo Ofisi ya Msajili, Bodi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(iv) Inaainisha taratibu na ngazi za usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi ya Wilaya, Mkoa, Taifa na Kimataifa;

(v) Inaainisha vyombo vya utatuzi wa migogoro ambavyo ni Msajili, Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Waziri mwenye dhamana;

(vi) Inampa mamlaka Msajili kuteua Wasajili Wasaidizi ambao watasaidia katika jukumu la uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vii) Kutoa wajibu wa kuwasilisha taarifa za mwaka za Mashirika;

(viii) Kutoa mamlaka kwa Waziri kutunga Kanuni za Usimamizi wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini;

(ix) Kuboresha tafsiri ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuongeza kwenye tafsiri hiyo maneno "shirika lisilogawana faida" lililoundwa kwa lengo la kusaidia jamii;

(x) Kuweka utaratibu wa kusajili Mashirika ya Kimataifa ambao ni pamoja na: kuwasilisha cheti cha usajili kutoka nchi liliposajiliwa Shirika, katiba na muhtasari wa wanachama waanzilishi wa Shirika wakiwemo watanzania wasiopungua wawili. Mashirika haya yanaelekezwa kujengea uwezo Mashirika ya ndani pamoja na kuheshimu mila na desturi za jamii ya kitanzania kwa mujibu wa Kifungu cha 33;

(xi) Kuyapa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali utu wa kisheria "legal personality";

(xii) Kuongeza masharti ya ukomo wa wajumbe wa Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwa ni pamoja na kufariki, kutiwa hatiani kwa kosa la jinai na kuthibitika kutokuwa na akili timamu;

(xiii) Kuweka wigo utakaowezesha Mashirika hayo kuwa na tafsiri pana inayotofautisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Taasisi nyingine. Kwa mujibu wa tafsiri mpya iliyotolewa kwenye kifungu 3 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023 imetambua Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yatakayojisajili chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa ni yale tu yanayolenga kunufaisha jamii na siyo wanachama wake. Aidha, tafsiri hiyo imeongeza Taasisi za Kijamii yaani 'CBOs' kuwa sehemu ya taasisi zitakazosimamiwa na Sheria hii;

(xiv) Kifungu cha 4 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023 kimelenga kumwongezea majukumu ya kisheria Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili endapo kutatokea ukiukwaji wa taratibu za kisheria aweze kuchukua hatua za kusitisha shughuli za Taasisi husika wakati akisubiri maamuzi ya Bodi. Vilevile, umetolewa muda wa notisi wa siku 30 kabla ya hatua hiyo kuchukuliwa. Aidha, kupitia kifungu hiki Msajili atafanya ufuatiliaji wa

taarifa za kazi kila robo mwaka na hivyo kuboresha ufuatiliaji na ukusanyaji wa taarifa za fedha na vyanzo vya mapato na matumizi ya rasilimali kwa kila robo mwaka ili kurahisisha uandaaji wa taarifa za mwaka; na

(xv) Kumpa mamlaka Msajili kwa mujibu wa kifungu cha 5 kufanya kazi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usimamizi wa Sheria.

**Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia Kanuni Na. 609 ya mwaka 2018**

Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023 imetungiwa Kanuni mbalimbali zikiwemo Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zilizotangazwa kwenye Tangazo la Serikali Na. 609 za mwaka 2018. Kanuni hizi ndiyo zinatoa ufafanuzi wa utekelezaji wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhusu uwazi na uwajibikaji wa fedha. Aidha, kupitia Kanuni hizo Serikali iliboresha misingi ya uwazi na uwajibikaji wa fedha za Mashirika hayo ili kuhakikisha zinawafikia wanufaika wa miradi inayotekelezwa na kuweka

utaratibu madhubuti wa uzingatiaji wa taratibu za kifedha za mapato, matumizi na manunuzi kwenye Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kama ifuatavyo: -

(i) Kuweka utaratibu wa kupokea na kuchambua mikataba mbalimbali ya fedha za wafadhili kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kutoa kibali cha matumizi ya fedha husika kwenye afua zilizoelezwa kwenye mkataba ikilinganishwa na malengo ya Mashirika husika;

(ii) Kuweka utaratibu wa kuwawezesha wanufaika wa miradi kutambua thamani halisi ya miradi iliyofadhiliwa na Mashirika husika kwenye maeneo yao;

(iii) Kuweka masharti ya kutangaza fedha zilizotumiwa na Mashirika hayo kwenye miradi ya maendeleo;

(iv) Kuimarisha uzingatiaji wa taratibu za kifedha; na

(v) Kudhibiti uingiaji wa mikataba ya ufadhili inayokinzana na Sheria za nchi.

**Mafanikio Yaliyopatikana Kutokana na Mabadiliko Yaliyofanyika Kupitia Kanuni Na. 609 ya mwaka 2018 na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.**

Mafanikio mbalimbali yamepatikana kufuatia mabadiliko yaliyofanyika kupitia Kanuni Na. 609 ya mwaka 2018 na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

(i) Kuimarika kwa misingi ya uwazi na uwajibikaji ambapo kwa sasa Mashirika yamekuwa yakiwasilisha mikataba/makubaliano yao ya ufadhili ambayo pamoja na mambo mengine inaainisha mtoaji wa fedha/rasilimali; kiasi cha fedha, wanufaika na lengo la matumizi ya fedha hizo;

(ii) Kuwezesha wanufaika wa miradi kupata taarifa mbalimbali za miradi inayotekelezwa na Mashirika katika maeneo yao hali ambayo inaweka bayana mradi uliotekelezwa ikilinganishwa na thamani ya fedha na

kurahisisha utekelezaji wa miradi kwa manufaa ya umma badala ya maslahi binafsi;

(iii) Kuwezesha Serikali kuchambua mikataba ya fedha za ufadhili na kuainisha rasilimali fedha iliyopitia kwenye Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na miradi mbalimbali ya kijamii iliyopatiwa ufadhili kupitia mikataba hiyo kwa lengo la kutambua mchango wa Mashirika hayo na kuhuishwa kwenye pato la Taifa;

(iv) Kuimarika kwa udhibiti na usimamizi wa miradi inayotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali iliyoainishwa kwenye mikataba na kuhakikisha inawafikia wanufaika kulingana na malengo ya Mashirika;

(v) Kuwa na tafsiri pana ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuweka wigo unaotofautisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Taasisi nyingine kama Makampuni, Vyama, Taasisi za kidini, Jumuiya na Benki Jamii 'Village Community Banks' (VICOBA);

(vi) Kuimarisha usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na hivyo kuongezeka kwa makusanyo ya mapato yanayotokana na ada mbalimbali zinazolipwa na Mashirika haya kila mwaka; na

(vii) Kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuzingatia matakwa ya Sera, Sheria, Kanuni na taratibu za nchi.

**Changamoto**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na marekebisho mbalimbali ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kumekuwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: -

**(i) Muingiliano na Mgongano wa Kiutendaji na Kiuratibu**

Baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kuwa na mgongano katika uratibu wa Mashirika hayo kutokana na vigezo mbalimbali vya kitaalam na hivyo kupelekea kukosekana kwa uratibu wa pamoja wa shughuli za Mashirika.

### (ii) Utegemezi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa Wafadhili

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali mengi yamekuwa hayana miradi ya kujiingizia kipato, badala yake yamekuwa yakitegemea zaidi fedha za ufadhili hususan ufadhili wa nje. Hali hii inayafanya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza miradi kwa kufuata matakwa ya Wafadhili badala ya malengo na vipaumbele vya nchi. Utegemezi huu pia unasababisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupenyeza agenda hasi katika mipango ya nchi na miradi kutokuwa endelevu.

### (iii) Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Mengi Kujikita Maeneo ya Mijini

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali mengi yamekuwa yakijielekeza kufanya kazi zake maeneo ya mjini ingawa maeneo hayo hayana changamoto kubwa kama ilivyo maeneo ya vijijini. Hali hii imetokana na wafadhili kuainisha maeneo ambayo kimsingi wako tayari kutoa fedha.

### (iv) Ukosefu wa Misingi ya Uwazi na Uwajibikaji

Baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekosa uwazi na uwajibikaji katika utendaji kazi kwa kutotoa taarifa za utekelezaji wa miradi kwa jamii zinazohudumiwa katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hali hii imekuwa ikileta taswira mbaya ya Sekta hii miongoni mwa jamii na kuyafanya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuonekana yanajinufaisha yenyewe kupitia matatizo yanayozikabili jamii tofauti na malengo yaliyokusudiwa. Ukosefu wa uwazi pia umesababisha baadhi ya Mashirika kutakasisha Fedha Haramu, kutumia jina la nchi vibaya na kutoa taarifa zinazopotosha jamii.

### (v) Kutotumika kwa Utaalam katika Utekelezaji wa Afua

Baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakitekeleza shughuli zake kwa kutumia uzoefu wa Mashirika mengine badala ya kutumia utaalam wakati wa upangaji wa shughuli za Mashirika hayo, na hivyo kutekeleza afua zinazofanana katika eneo moja na kufanya rasilimali kutumika pasipokuwa na tija. Hali hii imefanya uwepo wa mrundikano wa rasilimali fedha na huduma sehemu chache na kuacha sehemu nyingine za nchi bila huduma.

**Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto**

Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imepanga mikakati ifuatayo: -

(i) Kuandaa mwongozo huu wa uratibu wa pamoja wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kati ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(ii) Kuhamasisha Mashirika kubuni miradi endelevu ili kuyawezesha kujiendesha kama ilivyoainishwa katika Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2022/23 – 2026/27;

(iii) Kuimarisha ufuatiliaji wa fedha za miradi zinazopitia kwenye Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(iv) Kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanatekeleza majukumu kulingana na malengo yao na vipaumbele vya Taifa;

(v) Kuwezesha usajili na upatikanaji wa taarifa mbalimbali kwa njia ya kielektroniki kupitia mfumo wa usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(vi) Kuendelea kutathmini vihatarishi kwa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuzuia madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi mabaya ya vyanzo vya fedha;

(vii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali; na

(viii) Kuimarisha ushirikiano kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuwezesha uratibu mzuri wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

## SURA YA TATU: MAJUKUMU YA WIZARA, IDARA NA TAASISI ZA SERIKALI, SEKRETARIETI ZA MIKOA, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA, BARAZA LA TAIFA LA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NaCoNGO), SEKTA BINAFSI NA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

### Utangulizi

Mwongozo huu umeainisha majukumu ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Majukumu haya yameainishwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamiii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambayo ni Wizara yenye dhamana ya Sera na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mtaa (OR - TAMISEMI) ikiwa ni Wizara inayosimamia utekelezaji wa Sera katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Wizara ya Fedha kama msimamizi mkuu wa Sera na Sheria za fedha za Umma na miradi ya maendeleo nchini; na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama msimamizi wa Sera na Sheria za Ardhi nchini. Aidha, katika kuboresha huduma za uratibu wa Mashirika haya Mwongozo pia umeainisha majukumu ya Wizara za Kisekta, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Majukumu yaliyoainishwa, yatasaidia kukuza ushirikiano baina ya Serikali na wadau wa sekta hii, kuimarisha misingi ya uwazi na uwajibikaji na kuimarisha upatikanaji wa taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa wadau wengine wa sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Mwaka 2001 na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023;

(ii) Kuimarisha mfumo wa Kitaasisi wa kubadilishana taarifa kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuwezesha mchango wa Mashirika hayo kutambuliwa na Serikali;

(iii) Kusimamia uratibu wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini;

(iv) Kuratibu utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuhakikisha kuwa unakuwa na manufaa kwa nchi na jamii kwa kuzingatia vipaumbele vya maendeleo ya Taifa;

(v) Kusajili na kutunza rejista ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(vi) Kutunza kumbukumbu na taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(vii) Kuchambua taarifa za utekelezaji za robo mwaka, taarifa za utekelezaji nataarifa za ukaguzi za mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(viii) Kuchambua taarifa za utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka OR -TAMISEMI;

(ix) Kuandaa taarifa ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya nchi;

(x) Kuteua Maafisa wa Serikali (Wasajili Wasaidizi) ambao watakuwa wanatekeleza majukumu yao chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(xi) Kuteua Maafisa Waratibu wa Madawati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, na Sekta Binafsi

ambao wataratibu masuala ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika taasisi hizo;

(xii) Kujenga uwezo kwa Wasajili Wasaidizi, Waratibu wa Madawati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pamoja na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuweza kuboresha utendaji kwa kufuata Sheria, Kanuni, taratibu na maadili ya nchi;

(xiii) Kujenga uhusiano kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(xiv) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na ada za mwaka, ada ya upekuzi na ada ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(xv) Kuhakikisha kuwa mikataba ya ufadhili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inawasilishwa ili kujenga dhana ya uwazi na uwajibikaji;

(xvi) Kuimarisha mfumo wa usajili wa kielektroniki ili kurahisisha uratibu na usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(xvii) Kutoa elimu kwa umma juu ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; na

(xviii) Kutekeleza majukumu mengine ya kisera kama yatakavyojitokeza.

**Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI)**

OR - TAMISEMI itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kusimamia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi ya Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) Kuwezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutambua fursa na vipaumbele vya maendeleo vilivyopo katika mamlaka husika ili kuepuka Mashirika kutekeleza miradi inayofanana katika eneo moja;

(iii) Kuimarisha mfumo wa Kitaasisi wa ubadilishanaji wa taarifa kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), na Sekta Binafsi ili kuwezesha mchango wa Mashirika hayo kutambuliwa na Serikali;

(iv) Kuhakikisha Wasajili Wasaidizi wanahuisha taarifa na kumbukumbu za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyopo katika maeneo yao;

(v) Kuteua Afisa atakayeratibu dawati la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wizara;

(vi) Kuhakikisha kuwa shughuli zote za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zinaratibiwa na Afisa dawati aliyeteuliwa;

(vii) Kuhakikisha kuwa Wasajili Wasaidizi wanatoa taarifa ya awali kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali juu ya migogoro ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inayotokea ndani ya mamlaka zao;

(viii) Kutoa maelekezo kwa Wasajili Wasaidizi katika kuwezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza miradi katika maeneo yao kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023;

(ix) Kuwasilisha taarifa kila robo mwaka kuhusu utendaji wa Mashirika Yasiyoya Kiserikali kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(x) Kuhakikisha vikao vya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali vinaketi na taarifa zinafungamanishwa na vikao rasmi vya Serikali kuanzia ngazi ya msingi; na

(xi) Kutoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa kutoa nakala ya barua ya utambulisho wa miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa Makatibu Tawala wa Wilaya.

**Majukumu ya Afisa Dawati katika Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

(i) Kuratibu utoaji wa barua za utambulisho wa miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inayoenda kutekelezwa katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) Kuhakikisha kila Shirika linalopewa barua ya utambulisho wa mradi lina kibali cha mkataba wa ufadhili kutoka kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(iii) Kuratibu masuala ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayoshughulikiwa na waratibu wa Afya, Ustawi wa jamii na Lishe, Elimu pamoja na idara nyingine hasa vikao vya kitaalamu vya kupitia miradi inayoenda kutekelezwa;

(iv) Kuratibu na kuwa katibu wa vikao vya waratibu wa madawati ya Afya, Ustawi wa jamii, na Lishe na Elimu na mengineyo yote katika kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kila robo mwaka;

(v) Kuhakikisha kwamba malengo, afua na miradi inayotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaendana na Katiba za Mashirika yao, Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Sheria nyingine za nchi;

(vi) Kuhakikisha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi zinazofanana, yanatandaa na hayafanyi kazi eneo moja la utekelezaji wa mradi;

(vii) Kufatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi nchini; na

(viii) Kutekeleza majukumu mengine ya kisera kama itakavyoelekezwa na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

**Wizara ya Fedha**

Wizara ya Fedha itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha kuwa fedha zinazoingia kwenye Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kupitia Mikataba ya ufadhili zinazingatia matakwa ya Kanuni ya 609 ya mwaka 2018 inayohusu uwazi na uwajibikaji wa kifedha katika Mashirika Yasiyo ya kiserikali;

(ii) Kuweka kifungu maalumu kwenye mikataba mama '*Bilateral Agreements*' inayonufaisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuzitaka Nchi husika kutaja Mashirika yatakayonufaika kupitia mikataba hiyo;

(iii) Kubainisha orodha ya Mashirika yanayonufaika kupitia Mikataba mama '*Bilateral Agreements*' wakati wa kuingia mkataba au baada ya kukamilika mchakato shindanishi wa kuyapata Mashirika hayo na kuiwasilisha kwa ajili ya kupata kibali cha Msajili;

(iv) Kubainisha orodha ya Mashirika yaliyopitisha mikataba yake ya ufadhili moja kwa moja Hazina na kuwasilisha mikataba hiyo kwa Msajili kwa ajili ya kupata kibali, kuchambuliwa na kufuatilia utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa;

(v) Kuweka utaratibu wa kubadilishana taarifa kila robo mwaka na/au kila inapohitajika kati ya Dawati la Fedha za nje la Wizara ya Fedha na Dawati la uratibu wa mikataba ya fedha za wafadhili kwenye Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhusu fedha za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuwezesha mchango wa kifedha wa Mashirika hayo kutambuliwa na Serikali;

(vi) Kuratibu mikataba ya ufadhili yenye maslahi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kutunza kumbukumbu zake na kupata maoni ya Msajili kabla ya kuwekwa saini;

(vii) Kushirikiana na Ofisi ya Msajili katika kuhakikisha mifumo iliyopo ya kielektroniki inaunganishwa ili kurahisisha ufuatiliaji na upashanaji taarifa kuhusu mikataba ya ufadhili inayonufaisha Mashirika hayo;

(viii) Kuweka utaratibu wa kuratibu Mashirika yanayopata fedha na kuzigawa kwenye Mashirika mengine "grantors";

(ix) Kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa ubadilishanaji wa taarifa za fedha na utekelezaji kati ya Wizara za Kisekta na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuwezesha mchango wa Mashirika hayo kutambuliwa na Serikali; na

(x) Kuteua Afisa atakayeratibu dawati la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wizara.

**Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu(FIU) kilicho chini ya Wizara hiyo kitakuwa na majukumu yafuatayo:**

(i) Kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuhifadhi takwimu za Mashirika yaliyosajiliwa nchini kupitia mfumo wa takwimu wa taifa (NASMS);

(ii) Kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuhakikisha kuwa Mashirika yanakuwa na Sera za ndani madhubuti zitakazohakikisha kuwa Mashirika hayatumiki kufadhili ugaidi ndani na nje ya nchi;

(iii) Kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoa elimu kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhusiana na udhibiti wa utakasishaji Fedha Haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi;

(iv) Kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoa miongozo ya udhibiti ufadhili wa ugaidi ili kutambua na kubaini viashiria hatarishi vya ufadhili wa ugaidi;

(v) Kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuratibu ufanyaji wa tathmini ya viashiria hatarishi vya ufadhili wa ugaidi katika sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kushauri namna bora ya kukabiliana navyo;

(vi) Kuteua Afisa atakayeratibu dawati la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu(FIU) na

(vii) Kubadilishana taarifa zinazohusu usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yasitumike kufadhili ugaidi.

**Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 20(2) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023, Shirika Lisilo la Kiserikali lililosajiliwa lina utu wa kisheria "legal personality" na hivyo kuwa na uwezo wa kushtaki, kushtakiwa, kumiliki mali zinazohamishika na zisizohamishika, kuuza na kununua vitu mbalimbali kwa jina la Shirika. Hivyo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kabla ya Shirika kumilikishwa ardhi ni lazima kujiridhisha na kuhakikisha kuwa Shirika limesajiliwa kisheria, liko hai na lina cheti halali cha usajili;

(ii) Kuhakikisha kuwa ardhi inatolewa kwa jina la shirika na si la mtu binafsi;

(iii) Kuhakikisha kuwa Shirika Lisilo la Kiserikali linalokabidhiwa ardhi linazingatia Sera, Sheria, Kanuni na taratibu za umiliki wa ardhi bila kuathiri masharti yaliyowekwa chini ya Sheria ya Ardhi kuhusu umiliki wa ardhi kwa wageni;

(iv) Kuhakikisha kuwa kabla ya kuingia makubaliano au mikataba na Shirika Lisilo la Kiserikali katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu Mashirika hayo, Wizara iwasiliane na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kupata taarifa sahihi za Shirika husika;

(v) Kuwasiliana na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kila inapobainika Shirika linakiuka taratibu za utendaji kazi wake ikiwa ni pamoja na kujihusisha na vitendo vinavyokiuka Sheria za nchi, mila na desturi;

(vi) Kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa ubadilishanaji wa taarifa kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika

Yasiyo ya Kiserikali ili kuwezesha mchango wa Mashirika hayo kutambuliwa na Serikali;

(vii) Kusimamia vigezo vya kitaalam kwa kutoa idhini kwa Mashirika yanayojihusisha na sekta ya ardhi ili kulinda maslahi ya Nchi;

(viii) Kuwasiliana na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pale ambapo itabainika kuwa shirika linataka kuuza ardhi inayomilikiwa kwa jina la shirika na kwa manufaa ya wanufaika;

(ix) Kuteua Afisa atakayeratibu dawati la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wizara; na

(x) Kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pale inapobaini vitendo/viashiria vya uwepo wa shughuli za shirika kuwa kinyume na Sheria na kuzorotesha/kuhatarisha ulinzi, ustawi nausalama wa Nchi.

**Wizara za Kisekta**

Wizara za Kisekta zitakuwa na majukumu yafuatayo: -

(xi) Kabla ya kuanza kufanya kazi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhakikisha kuwa Shirika limesajiliwa kisheria, liko hai na lina cheti halali cha usajili;

(xii) Kuhakikisha kuwa fedha za Mashirika zinatumika kwenye miradi na afua zilizokusudiwa na zenye matokeo chanya kwa jamii kwa kuzingatia malengo ya usajili wake kama yalivyoainishwa kwenye Katiba yake;

(xiii) Kuhakikisha kuwa utendaji kazi wa kila Shirika Lisilo la Kiserikali unazingatia Sera, Sheria, Kanuni na taratibu za nchi;

(xiv) Kuhakikisha kuwa kabla ya kuingia makubaliano au mikataba na Shirika Lisilo la Kiserikali katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu Mashirika hayo, Wizara za Kisekta ziwasiliane na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kupata taarifa sahihi za Shirika husika;

(xv) Kuwasiliana na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kila inapobainika kuwa Shirika linakiuka taratibu za utendaji kazi wake ikiwa ni pamoja na kujihusisha na vitendo vinavyokiuka Sheria za nchi, mila na desturi;

(xvi) Kuwezesha Mashirika kutambua fursa na vipaumbele vya maendeleo vilivyopo katika sekta husika pamoja na kutekeleza miradi yake kwa kuzingatia vigezo vya kitaalam katika Sekta hiyo ili kuepuka miradi inayotekelezwa chini ya viwango na isiyozingatia utaalam wa kisekta;

(xvii) Kuwezesha Mashirika kupata utambulisho kutoka katika Wizara ya Kisekta inayohusika na eneo hilo;

(xviii) Kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa ubadilishanaji wa taarifa za fedha na utekelezaji kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuwezesha mchango wa Mashirika hayo kutambuliwa na Serikali;

(xix) Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wizara za Kisekta kuandaa Sura ya Kisekta (Sector Profile) ili kuweka wazi maeneo yenye mahitaji kwa lengo la kuondoa mrundikano;

(xx) Wizara za Kisekta zisimamie vigezo vya kitaalam kulinda maslahi ya nchi;

(xxi) Kuteua Maafisa watakaoratibu madawati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wizara;

(xxii) Kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pale wanapobaini vitendo/viashiria vya uwepo wa shughuli za shirika kuwa kinyume na Sheria na kuzorotesha/kuhatarisha ulinzi, ustawi na usalama wa Nchi;

(xxiii) Kuhakikisha kuwa Shirika linatekeleza afua zinazoendana na vipaumbele vya nchi; na

(xxiv) Kuhakikisha kuwa Mashirika hayaendi kinyume na Ibara 41 (1) ya Mkatabawa Vienna kuhusu Uhusiano wa Kidiplomasia wa mwaka 1961 unaozuia nchi na wadau wa nje kuingilia masuala ya ndani ya nchi.

**Idara na Taasisi za Serikali**

Idara na Taasisi za Serikali zitakuwa na majukumu yafuatayo,

(i) Kabla ya kuanza kufanya kazi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhakikisha kuwa Shirika limesajiliwa kisheria, liko hai na lina cheti halali cha usajili;

(ii) Kuhakikisha kuwa fedha za Mashirika zinatumika kwenye miradi na afua zilizokusudiwa na zenye matokeo chanya kwa jamii kwa kuzingatia malengo ya usajili wake kama yalivyoainishwa kwenye Katiba yake;

(iii) Kuhakikisha kuwa utendaji kazi wa kila Shirika Lisilo la Kiserikali unazingatia Sera, Sheria, Kanuni na taratibu za nchi;

(iv) Kuhakikisha Taasisi ina kuwa na Dawati la Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na linaratibiwa na Afisa Mratibu aliyeteuliwa na Mtendaji Mkuu wa Taasisi;

(v) Kuhakikisha kuwa kabla ya kuingia makubaliano au mikataba na Shirika Lisilo la Kiserikali katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu

Mashirika hayo, Idara na Taasisi za Serikali ziwasiliane na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kupata taarifa sahihi za Shirika husika;

(vi) Kuwasiliana na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kila inapobainika kuwa Shirika linakiuka taratibu za utendaji kazi wake ikiwa ni pamoja na kujihusisha na vitendo vinavyokiuka Sheria za nchi, mila na desturi;

(vii) Kuwezesha Mashirika kutambua fursa na vipaumbele vya maendeleo vilivyopo katika sekta husika pamoja na kutekeleza miradi yake kwa kuzingatia vigezo vya kitaalam katika Sekta hiyo ili kuepuka miradi inayotekelezwa chini ya viwango na isiyozingatia utaalam wa kisekta;

(viii) Kuwezesha Mashirika kupata utambulisho kutoka katika Taasisi ya Serikali inayohusika na eneo hilo;

(ix) Kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa ubadilishanaji wa taarifa za fedha na utekelezaji kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Taasisi ya Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuwezesha mchango wa Mashirika hayo kutambuliwa na Serikali;

(x) Idara na Taasisi za Serikali zisimamie vigezo vya kitaalam kulinda maslahi ya nchi;

(xi) Kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pale wanapobaini vitendo/viashiria vya uwepo wa shughuli za shirika kuwa kinyume na Sheria na kuzorotesha/kuhatarisha ulinzi, ustawi na usalama wa Nchi;

(xii) Kuhakikisha kuwa Shirika linatekeleza afua zinazoendana na vipaumbele vya nchi; na

(xiii) Kuhakikisha kuwa Mashirika hayaendi kinyume na Ibara 41 (1) ya Mkatabawa Vienna kuhusu Uhusiano wa Kidiplomasia wa mwaka 1961 unaozuia nchi na wadau wa nje kuingilia masuala ya ndani ya nchi.

**Wakuu wa Mikoa na Sekretarieti za Mikoa**

Wakuu wa Mikoa na Sekretarieti za Mikoa kupitia Makatibu Tawala wa Mikoa na Wasajili Wasaidizi katika Mikoa (Maafisa Maendeleo ya Jamii) watakuwa na majukumu yafuatayo:

**Wakuu wa Mikoa**

(i) Wakuu wa Mikoa watakuwa Wenyeviti wa vikao vya robo mwaka, mwaka na vikao vyote vya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Mikoa vitakavyoratibiwa na Msajili Msaidizi Mkoa kwa kushirikiana na Mjumbe wa NaCoNGO Mkoa pamoja na wajumbe wa Sekretarieti;

(ii) Mkuu wa Mkoa anaweza kuteua/kukasimisha Uenyekiti wa vikao vya robo mwaka, mwaka na vikao vyote vya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa Kiongozi yoyote pindi anapokuwa na majukumu mengine ya Kitaifa;

(iii) Kutumia majukwaa ya Mikoa kutoa taarifa kwa wadau wengine kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Mkoa;

(iv) Kuwahamasisha wanufaika wa miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuilinda miradi hiyo, kuitumia kujiletea maendeleo na kuifanya miradi hiyo kuwa endelevu;na

(v) Kuhamasisha Mashirika kubuni miradi endelevu ili kuyawezesha kujiendesha na kuongoza shughuli za utafutaji rasilimali fedha za Mashirika katika Mkoa.

**Makatibu Tawala wa Mikoa**

(i) Makatibu Tawala watayatambulisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Makatibu Tawala Wilaya watapewa nakala ya barua ya utambulisho;

(ii) Kuelekeza na kuhakikisha vikao vya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali vinaketi na taarifa zake zinafungamanishwa katika vikao rasmi vya Serikali ambavyo ni Baraza la Ushauri la Mkoa(RCC), Baraza la Ushauri

la Wilaya (DCC), Baraza la Maendeleo la Tarafa (BMT) na Baraza la Maendeleo la Kata (WDC);

(iii) Kuteua wajumbe wa Sekretarieti ya Mkoa itakayokuwa wajumbe wa Idara zinazotekeleza kazi za Wizara za kisekta ambapo Msajili Msaidizi wa Mkoa atakuwa Katibu ili kuratibu vikao na shughuli za Mashirika katika Mkoa;

(iv) Kutoa maelekezo juu ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(v) Kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwemo utengaji wa bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini kama zilivyoainishwa katika mwongozo huu;

(vi) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi kwa kutembelea maeneo ya miradi na kuhamasisha ushindani miongoni mwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(vii) Kufuatilia na kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Kamati ya Menejimenti ya Mkoa katika vipindi vya robo, nusu na mwaka.

**Wasajili Wasaidizi katika Mikoa**

(i) Kupokea na kupitia maombi ya awali ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) Kupitia nyaraka za usajili za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuhakikisha kuwa nyaraka hizo zimekamilika na hivyo kutoa barua ya utambulisho wa Shirika linalotaka kuanzishwa kwenda kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(iii) Kuainisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya pamoja na kutunza kumbukumbu na taarifa za Mashirika hayo;

(iv) Kuhakikisha kwamba malengo, afua na miradi inayotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaendana na Katiba za Mashirika yao, Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Sheria nyingine za nchi;

(v) Kuhakikisha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi zinazofanana, yanatandaa na hayafanyi kazi eneo moja la utekelezaji wa

mradi;Kuhakikisha kwamba Shirika linalofanya kazi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya linawajibika kwa watu linaowahudumia kwa kutangaza miradi na fedha ambazo zitatumika katika kutekeleza miradi;

(vi) Kufatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya;

(vii) Kuratibu taarifa za robo ufuatiliaji za Wasajili Wasaidizi wa Halmashauri na kuziwakilisha kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(viii) Wasajili wasaidizi watakuwa Waratibu na Makatibu wa vikao vya robo mwaka, mwaka na vikao vyote vya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; na

(ix) Kutekeleza majukumu mengine ya kisera kama itakavyoelekezwa na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

**Wakuu wa Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Wakuu wa Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wasajili Wasaidizi katika ngazi za Halmashauri, watakuwa na majukumu yafuatayo;

**Wakuu wa Wilaya**

(i) Wakuu wa Wilaya watakuwa Wenyeviti wa vikao vya robo mwaka, mwaka na vikao vyote vya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali vitakavyoratibiwa na Msajili Msaidizi kwa kushirikiana na Wajumbe wa NaCoNGO katika Halmashauri na Wilaya;

(ii) Mkuu wa Wilaya anaweza kuteua/kukasimisha Uenyekiti wa vikao vya robo mwaka, mwaka na vikao vyote vya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa Kiongozi yoyote pindi anapokuwa na majukumu mengine ya Kitaifa;

(iii) Kutumia majukwaa ya Wilaya kutoa taarifa kwa wadau wengine kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wilaya;

(iv) Kuwahamasisha wanufaika wa miradi ya Mashirika Yasiyo yaKiserikali kuilinda miradi hiyo, kuitumia kujiletea maendeleo na kuifanya miradi hiyo kuwa endelevu;

(v) Kusitisha kwa muda kibali cha utekelezaji wa mradi kwa Shirika Lisilo la Kiserikali litakalobainika kufanya shughuli zake kinyume na Sheria, mila na desturi za kitanzania katika eneo lake; na

(vi) Kuhamasisha Mashirika kubuni miradi endelevu ili kuyawezesha kujiendesha na kuongoza shughuli za utafutaji rasilimali fedha za Mashirika katika Wilaya.

**Makatibu Tawala wa Wilaya**

(i) Kutoa maelekezo juu ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(ii) Kuhakikisha vikao vya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali vinaketi na taarifa zake zinafungamanishwa katika vikao rasmi vya Serikali ambavyo ni Baraza la Maendeleo la Tarafa (BMT) na Baraza la Maendeleo la Kata (WDC);

(iii) Kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika vikao vya Kamati ya Ulinzi na Usalama;

(iv) Kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwemo utengaji wa bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini kama zilivyoainishwa katika mwongozo huu; na

(v) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi kwa kutembelea maeneo ya miradi na kuhamasisha ushindani miongoni mwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri**

(i) Kuhakikisha vikao vya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali vinaketi na taarifa zake zinafungamanishwa katika vikao rasmi vya Serikali ambavyo ni Vikao cha Menejimenti ya Halmashauri (CMT), Baraza la Ushauri la Wilaya (DCC), Baraza la Maendeleo la Tarafa (BMT) na Baraza la Maendeleo la Kata (WDC);

(ii) Kujenga uelewa wa Wakuu wa Idara na Baraza la Madiwani juu ya faida na umuhimu wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(iii) Kuratibu Kikao cha Menejimenti ya Halmashauri katika kupendekeza bajeti kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathimini kwa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(iv) Kutoa maelekezo muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(v) Kuteua wajumbe wa Sekretarieti ya Halmashauri itakayokuwa na wajumbe wa Idara zinazotekeleza kazi za Wizara za kisekta ambapo Msajili Msaidizi wa Halmashauri atakuwa Katibu ili kuratibu vikao na shughuli za Mashirika katika Halmashauri; na

(vi) Kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika vikao vya Kamati ya Ulinzi na Usalama.

**Wasajili Wasaidizi katika Halmashauri**

(i) Kuhakikisha kuwa Shirika Lisilo la kiserikali linalofanya kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa limesajiliwa chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023 na kutambuliwa kwa cheti naKatiba yake;

(ii) Kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa ubadilishanaji wa taarifa kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuwezesha mchango wa Mashirika hayo kutambuliwa na Serikali;

(iii) Kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanafanya kazi kwa mujibu wa nyaraka zao za usajili na si vinginevyo kama ilivyoelekezwa na kifungu cha 32(1) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania;

(iv) Kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pale inapobaini vitendo/viashiria vya uwepo wa shughuli za shirika kuwa kinyume na Sheria na kuzorotesha/kuhatarisha ulinzi, ustawi na usalama wa nchi;

(v) Kuhakikisha kuwa Shirika linalotekeleza mradi/afua inayozidi fedha za kitanzania Shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) linawasilisha barua ya idhini kutoka kwa Msajili kulingana na Kanuni ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 609 ya mwaka 2018 kifungu cha kanuni 13 (b);

(vi) Kuhakikisha kuwa miradi/afua inayotekelezwa inazingatia vipaumbele vya maendeleo ya Taifa, inaleta tija kwa jamii na kutatua changamoto zinazolizunguka eneo la utekelezaji wa mradi;

(vii) Kufatilia taarifa za utekelezaji za robo mwaka pamoja na taarifa za utekelezaji na taarifa za ukaguzi za mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(viii) Wasajili wasaidizi watakuwa waratibu na makatibu wa vikao vya robo mwaka, mwaka na vikao vyote vya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(ix) Kuandaa taarifa zao za robo za ufuatiliaji, vikao vya robo na Jukwaa la Mwaka na kuwasilisha kwa Msajili Msaidizi wa Mkoa; na

(x) Kuandaa taarifa ya utekelezaji kuhusu utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kila robo mwaka na kuziwasilisha kwa Msajili na OR TAMISEMI kupitia fomu maalumu iliyoandaliwa.

**Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO)**

Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) limeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 27(1) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania. Majukumu ya Baraza katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni kama ifuatavyo:

(i) Kulinda na kusimamia maslahi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(ii) Kuyaunganisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Serikali na wadau wengine;

(iii) Kusimamia uratibu wa mienendo ya shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(iv) Kuyajengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(v) Kukusanya, kuchakata na kusambaza taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa ajili ya fursa mbalimbali;

(vi) Kuwa kiungo baina ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Serikali na wadau mbalimbali;

(vii) Kuimarisha uzingatiaji wa Sheria kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(viii) Kusambaza taarifa ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa;

(ix) Kuwakilisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

(x) Kusuluhisha migogoro baina ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wadau wengine;

(xi) Kuhamasisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kufanya shughuli zake kwa kufuata mila na desturi za Mtanzania;

(xii) Kutafuta rasilimali na kuhakikisha utandaa wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maeneo tofauti;

(xiii) Kuandaa majukwaa na Mkutano wa Mwaka wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; na

(xiv) Kuimarisha mitandao ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

**Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

**(i) Mashirika ya Kitaifa**

Ili kusimamia ipasavyo taratibu za uendeshaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini, Mashirika ya Kitaifa yanatakiwa kuzingatia masharti ya sheria na taratibu za nchi kwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kujisajili kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023 kabla ya kuanza shughuli yoyote ya shirika husika;

(ii) Kufanya kazi zao kwa mujibu wa nyaraka za usajili ikiwemo cheti cha usajili na Katiba kwa mujibu wa kifungu cha 32(1) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56;

(iii) Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhakikisha yanalinda maslahi ya Nchi ikiwa ni pamoja na kutii Sheria na kuheshimu mila na desturi za jamii ya

kitanzania kwa mujibu wa Kifungu cha 33 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023;

(iv) Kuwasilisha taarifa za robo mwaka na taarifa za mwaka za utekelezaji wa shughuli zake na taarifa ya fedha iliyokaguliwa kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wizara za Kisekta zinazosimamia afua za utekelezaji wa shirika hilo;

(v) Kutoa taarifa za fedha na vyanzo vya mapato na matumizi ya rasilimali kwa kila robo mwaka kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara za Kisekta zinazosimamia afua za utekelezaji wa shirika hilo na kwa wanufaika;

(vi) Mashirika yatakayopewa fedha na wafadhili yanapaswa kuwasilisha mikataba ya fedha za ufadhili kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wizara ya Fedha kwa mujibu wa Kanuni 609 ya mwaka 2018 kifungu cha kanuni 13 (b);

(vii) Kuhakikisha wanufaika wanashirikishwa ipasavyo katika uibuaji, upangaji na utekelezaji wa miradi ili kuwa na umiliki wa miradi hiyo;

(viii) Kuhakikisha Shirika linawasiliana na Wizara ya Kisekta ili kubaini maeneo yenye uhitaji na kupata mwongozo wa kisera kabla ya kuanza kutekeleza miradi/afua;

(ix) Kuzingatia mipango na vipaumbele vya Serikali katika kupanga mipango kazi yao ya mwaka;

(x) Kutumia fedha kwa kuzingatia dhamana ya fedha katika miradi inayosaidia jamii na sio kutumia fedha hizo kwa ajili ya gharama za uendeshaji;

(xi) Kuhakikisha yanazingatia Sheria za Nchi hasa zinazosimamia afua za utekelezaji mfano suala la utoaji wa elimu shuleni na kufanya tafiti mbalimbali nchini kwa kupata vibali vya mamlaka husika kama vile Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH);

(xii) Mashirika yote yanayopata fedha kupitia mikataba ya ufadhili iliyo chini ya Shilingi 20,000,000/= yanatakiwa kuwasilisha taarifa za miradi/afua

inayotekelezwa kwa Msajili, Sekretarieti za Mkoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, wanufaika wa miradi na Wizara za Kisekta zinazosimamia utekelezaji wa afua;

(xiii) Kutotumika katika kufanya ujasusi kwa nchi kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume na Sheria za nchi;

(xiv) Kutoa taarifa na takwimu sahihi kwa Wizara za Kisekta ili kurahisisha utendaji kazi na kuwezesha mamlaka nyingine za Serikali kupata taarifa kwa wakati pale zinapohitajika katika maandalizi ya mipango mbalimbali na masuala mengine ya kisera;

(xv) Kufanikisha utekelezaji wa Kanuni Na. 609 ya Mwaka 2018 inayohusu misingi ya uwazi na uwajibikaji wa kifedha katika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(xvi) Kuwasilisha kwa Msajili mikataba na makubaliano ya utekelezaji yaliyofikiwa baina ya Shirika Lisilo la kiserikali na Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi;

(xvii) Mashirika yanayopata fedha kutoka nchi marafiki au mashirika yenye hadhi ya kidiplomasia kuhakikisha kuwa misaada hiyo haiendi kinyume na Ibara 41 (1) ya Mkataba wa Vienna kuhusu Uhusiano wa Kidiplomasia wa mwaka 1961 unaozuia nchi na wadau wa nje kuingilia masuala ya ndani ya nchi;

(xviii) Kushirikisha Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uandaaji wa mipango yao ya kazi na kutoa taarifa za utekelezaji;

(xix) Kuzingatia masharti yaliyowekwa na Sheria ya kuzuia utakasishaji Fedha, Na. 12 ya mwaka 2006;

(xx) Mashirika yanayotekeleza miradi/afua za Kisekta mfano afya, elimu, ardhi, kilimo, mazingira, madini, maji na sekta nyingine zote kuhakikisha yanapata vibali vya mamlaka husika kabla ya kutekeleza afua hizo;

(xxi) Kuhakikisha Shirika linatumia fedha za ufadhili kutekeleza miradi ambayo haikinzani na mila, maadili, desturi na utamaduni wa mtanzania; na

(xxii) Kuhakikisha kila shirika linakuwa na Mpango Mkakati wa Uendelevu na sera za ndani za uendeshaji wa Shirika.

**(ii) Mashirika ya Kimataifa**

(i) Mashirika ya Kimataifa yana jukumu la kuyajengea uwezo Mashirika madogo ya Kitaifa kwa mujibu wa Kifungu cha 33(d)(i) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania;

(ii) Kuhakikisha wakati wa utekelezaji wa miradi kila Shirika la Kimataifa lina ofisi maeneo ya miradi Mikoani;

(iii) Kujisajili kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023 kabla ya kuanza shughuli yoyote ya shirika husika ikiwemo kuhakikisha Shirika linawasilisha cheti cha usajili kutoka nchi liliposajiliwa, Katiba na Muhtasari wa wanachama waanzilishi wa Shirika wakiwemo watanzania wasiopungua wawili;

(iv) Kuhakikisha Shirika linashiriki vikao vinavyoitishwa katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za mitaa ilipo miradi yao ili kupanga miradi pamoja na kuhakikisha wanufaika wanashirikishwa ipasavyo katika uibuaji, upangaji na utekelezaji wa miradi ili kuwa na umiliki wa miradi hiyo;

(v) Kufanya kazi zao kwa mujibu wa nyaraka za usajili ikiwemo cheti cha usajili na Katiba kwa mujibu wa kifungu cha 32(1) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56;

(vi) Kuhakikisha yanalinda maslahi ya Nchi ikiwa ni pamoja na kutii Sheria na kuheshimu Mila na Desturi za jamii ya Kitanzania kwa mujibu wa Kifungu cha 33 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023;

(vii) Kuwasilisha taarifa za robo mwaka na taarifa za mwaka za utekelezaji wa shughuli zake na taarifa ya fedha iliyokaguliwa kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wizara za Kisekta zinazosimamia afua za utekelezaji wa shirika hilo;

(viii) Kutoa taarifa za fedha na vyanzo vya mapato na matumizi ya rasilimali kwa kila robo mwaka kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara za Kisekta zinazosimamia afua za utekelezaji wa shirika hilo na kwa wanufaika;

(ix) Mashirika yatakayopewa fedha na wafadhili yanapaswa kuwasilisha mikataba ya fedha za ufadhili kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wizara ya Fedha kwa mujibu wa Kanuni 609 ya mwaka 2018 kifungu cha kanuni 13 (b);

(x) Kuhakikisha Shirika linawasiliana na Wizara ya Kisekta ili kubaini maeneo yenye uhitaji na kupata Mwongozo wa Kisera kabla ya kuanza kutekeleza miradi/afua;

(xi) Kuzingatia mipango na vipaumbele vya Serikali katika kupanga mipango kazi yao ya mwaka;

(xii) Kutumia fedha kwa kuzingatia dhamana ya fedha katika miradi inayosaidia jamii na sio kutumia fedha hizo kwa ajili ya gharama za uendeshaji;

(xiii) Kuhakikisha yanazingatia Sheria za Nchi hasa zinazosimamia afua za utekelezaji mfano suala la utoaji wa elimu shuleni na kufanya tafiti mbalimbali nchini kwa kupata vibali vya mamlaka husika kama vile Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH);

(xiv) Mashirika yote yanayopata fedha kupitia mikataba ya ufadhili iliyo chini ya Shilingi 20,000,000/= yanatakiwa kuwasilisha taarifa za miradi/afua inayotekelezwa kwa Msajili, Sekretarieti za Mkoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, wanufaika wa miradi na Wizara za Kisekta zinazosimamia utekelezaji wa afua;

(xv) Kutotumika katika kufanya ujasusi kwa nchi kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume na Sheria za nchi;

(xvi) Kutoa taarifa na takwimu sahihi kwa Wizara za Kisekta ili kurahisisha utendaji kazi na kuwezesha mamlaka nyingine za Serikali kupata taarifa kwa wakati pale zinapohitajika katika maandalizi ya mipango mbalimbali na masuala mengine ya kisera;

(xvii) Kufanikisha utekelezaji wa Kanuni Na. 609 ya Mwaka 2018 inayohusu misingi ya uwazi na uwajibikaji wa kifedha katika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(xviii) Kuwasilisha kwa Msajili mikataba na makubaliano ya utekelezaji yaliyofikiwa baina ya Shirika Lisilo la kiserikali na Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi;

(xix) Mashirika yanayopata fedha kutoka nchi marafiki au mashirika yenye hadhi ya kidiplomasia kuhakikisha kuwa misaada hiyo haiendi kinyume na Ibara 41 (1) ya Mkataba wa Vienna kuhusu Uhusiano wa Kidiplomasia wa mwaka 1961 unaozuia nchi na wadau wa nje kuingilia masuala ya ndani ya nchi;

(xx) Kuzingatia masharti yaliyowekwa na Sheria ya kuzuia utakasishaji Fedha, Na. 12 ya mwaka 2006;

(xxi) Mashirika yanayotekeleza miradi/afua za Kisekta mfano afya, elimu, ardhi, kilimo, mazingira, madini, maji na sekta nyingine zote kuhakikisha yanapata vibali vya mamlaka husika kabla ya kutekeleza afua hizo;

(xxii) Kuhakikisha Shirika linatumia fedha za ufadhili kutekeleza miradi ambayo haikinzani na mila, maadili, desturi na utamaduni wa Mtanzania; na

(xxiii) Kuhakikisha kila shirika linakuwa na Mpango Mkakati wa Uendelevu na sera za ndani za uendeshaji wa Shirika.

**Sekta Binafsi**

Sekta Binafsi kama wadau wa Serikali katika kuleta maendeleo nchini, zitakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kabla ya kuanza kufanya kazi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhakikisha kuwa Shirika limesajiliwa kisheria, liko hai na lina cheti halali cha usajili;

(ii) Kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa kwa Mashirika zinatumika kwenye miradi/afua zilizokusudiwa na zenye matokeo chanya kwa jamii;

(iii) Kuhakikisha kuwa kabla ya kuingia makubaliano au mikataba na Shirika Lisilo la Kiserikali katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu Mashirika hayo, Sekta binafsi zinawasiliana na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kupata taarifa sahihi za Shirika husika;

(iv) Kuwasiliana na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kila inapobainika kuwa Shirika linakiuka taratibu za utendaji kazi wake ikiwa ni pamoja na kujihusisha na vitendo vinavyokiuka Sheria, mila na desturi za nchi;

(v) Kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa ubadilishanaji wa taarifa kati ya Sekta Binafsi na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuwezesha mchango wa Mashirika hayo kutambuliwa na Serikali;

(vi) Kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama na kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pale wanapobaini vitendo/viashiria vya uwepo wa shughuli za Shirika kuwa kinyume na Sheria na kuzorotesha/kuhatarisha ulinzi, ustawi na usalama wa nchi;

(vii) Kuchangia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yaweze kutekeleza miradi/afuakwa kutegemea ufadhili wa ndani na kuondoa utegemezi wa ufadhili wa nje; na

(viii) Kuhakikisha kuwa Shirika linatekeleza miradi/afua zinazoendana na vipaumbele vya nchi.

## SURA YA NNE: MIKUTANO YA MAJADILIANO NA JAMII PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MILA NA DESTURI ZA KITANZANIA

### Mikutano ya Majadiliano na Jamii

Mwongozo huu utatekelezwa kwa kuzingatia Mpango na Mwongozo wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi 2022/23- 2025/26. Mwongozo huu unatoa tafsiri ya mikutano ya majadiliano na jamii ambayo inalenga kuwezesha wananchi kufahamu shughuli zinazofanywa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kupata mrejesho kutoka kwa wanufaika wa miradi na jinsi miradi hiyo inavyowagusa wananchi kutokana na huduma wanazopata. Aidha, majadiliano hayo husaidia kujua changamoto zinazowakabili kupitia miradi inayotekelezwa pamoja na kutafuta suluhisho la changamoto zitakazokuwa zimejitokeza na namna ya kuifanya miradi inayotekelezwa kuwa endelevu. Vilevile, Mikutano ya majadiliano na jamii husaidia kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kujenga mahusiano ya karibu na wananchi ili waweze kuwa na imani na Mashirika hayo na ushirikiano endelevu katika utekelezaji wa miradi.

### Uzingatiaji wa Mila na Desturi

Mwongozo huu utatekelezwa sambamba na Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii. Mwongozo huo unalenga kukuza na kuimarisha mila na desturi chanya zinazowezesha jamii kujenga mahusiano mazuri yenye kuleta heshima na yanayozingatia usawa wa kijinsia pamoja na kulinda haki za wanawake na watoto dhidi ya aina zote za vitendo vya ukatili ndani ya jamii. Aidha, kwa kutekelezwa sambamba na Mwongozo huu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yataweza kufanya shughuli zao kwa kufuata Mila na Desturi za Mtanzania.

# SURA YA TANO: UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MWONGOZO

## Utangulizi

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli zilioainishwa kwenye Mwongozo huu utahusisha upitiaji wa taarifa za utekelezaji za robo na mwaka, taarifa za fedha zilizokaguliwa, nyaraka, ziara kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kufanya mikutano kila robo mwaka, Majukwaa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na mikutano na wadau wa maendeleo, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ( NaCoNGO), Idara na Taasisi za Serikali na Sekta binafsi. Taarifa za kila robo mwaka zitatolewa mara baada ya kila kikao na taarifa ya mchango ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali itatolewa wakati wa Jukwaa la mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Taarifa za kila robo mwaka na mwaka mzima zitatolewa ili kuweka kumbukumbu za utekelezaji, mafanikio, changamoto na mapendekezo yatakayoboresha mazingira wezeshi ya uratibu kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

## Mpangilio wa Kitaasisi wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mpangilio wa kitaasisi wa ufuatiliaji na tathmini utahusisha mazingira ya kitaasisi yanayozingatia mifumo ya kitaasisi na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika utekelezaji wa mpango wa ufuatiliaji na tathmini. Kila Taasisi itahakikisha inatenga bajeti kwa ajili kuwezesha kazi za ufuatiliaji na tathmini ili kuangalia utekelezaji wa Mwongozo katika Taasisi husika. Aidha, Ufuatiliaji na tathmini wa Mwongozo huu utahusisha kubainisha viashiria ambavyo utendaji kazi wake utatathminiwa. Viashiria hivi vitafuatiliwa na kupimwa mara kwa mara kwa Wasajili Wasaidizi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuhakikisha malengo yanafikiwa na utekelezaji wa Mwongozo unaendelea.

## Mipango ya Mwaka ya Ufuatiliaji na Tathmini

Ili kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi wa mpangilio wa kitaasisi wa ufuatiliaji na tathmini, Majukwaa ya Mwaka ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, vikao vya wadau vya kisekta vitaratibiwa na Wizara yenye dhamana kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kila mwaka ili kufanya mapitio ya takwimu zilizokusanywa kuhusu viashiria mbalimbali vilivyoainishwa katika kupima maendeleo ya utekelezaji wa Mwongozo na

kuchukua hatua zozote muhimu na za haraka kwa ajili kurekebisha changamoto zitakazojitokeza.

## SURA YA SITA: HITIMISHO

Mwongozo huu ni kwa ajili ya kuimarisha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kujenga uelewa wa pamoja ili kuweza kwenda pamoja kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya Taifa kwa kuzingatia misingi ya uwazi na uwajibikaji. Mwongozo pia utasaidia kujenga ushirikiano katika utendaji na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali baina ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 kama ilivyofanyiwa marejeo 2023 pamoja na Kanuni zake. Hivyo, Mwongozo huu utatumika kama nyenzo na dira muhimu katika kuhakikisha kuwa lengo kuu la Mwongozo ambalo ni kuondoa muingiliano na mgongano wa kiutendaji linafikiwa. Aidha, Mwongozo huu utatumika bila kuathiri mifumo ya Serikali iliyopo.

## VIAMBATANISHO

**KIAMBATANISHO 1: VIASHIRIA VYA UTENDAJI KAZI KWA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**

**KIAMBATANISHO 2: VIASHIRIA VYA UTENDAJI KAZI KWA WASAJILI WASAIDIZI**

**KIAMBATANISHO NA. 2: VIASHIRIA VYA UTENDAJI KAZI KWA WASAJILI WASAIDIZI**

| Na. | LENGO | KIASHIRIA | MAELEZO | NJIA YA UPIMAJI | MUDA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kufanya vikao vinne (4) vya robo mwaka | Idadi ya Vikao vya robo mwaka vilivyofanyika chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa/Wilaya au Kiongozi aliyeteuliwa/ kukasimishwa na Mkuu wa Mkoa/Wilaya | Jumla ya vikao vya robo mwaka vilivyoratibiwa na Msajili Msaidizi | Kuhesabu vikao vya robo mwaka vilivyofanyika | Robo mwaka | Msajili Msaidizi, Msajili, Waratibu wa Madawati, NaCoNGO |
| 2 | Vikao rasmi vya Serikali vilivyofungamanisha taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Idadi rasmi ya vikao rasmi vya Serikali vilivyofungamanisha taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Jumla ya vikao rasmi vya Serikali vilivyofungamanisha taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Kuhesabu vikao rasmi vya Serikali vilivyofungamanisha taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Robo mwaka na Mwaka | Msajili Msaidizi, Msajili, Mratibu wa Dawati la NGOs TAMISEMI, NaCoNGO |
| 3 | Kufanya ziara za kutembelea Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuangalia utekelezaji wa miradi | Idadi ya Mashirika yaliyotembelewa | Jumla ya Mashirika yaliyotembelewa kwa robo mwaka | Kuhesabu Mashirika yaliyotembelewa katika nyaraka za taarifa za robo mwanka na mwaka | Robo mwaka | Msajili Msaidizi, Msajili, Waratibu wa Madawati, NaCoNGO |
| 4 | Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwasilisha taarifa za robo na mwaka na ulipaji wa ada kwa wakati | Idadi ya Mashirika yaliyowasilisha taarifa na kulipa ada | Asilimia ya Mashirika yaliyowasilisha taarifa na kulipa ada kwa wakati | Asilimia ya Mashirika yaliwasilsha taarifa za utendaji kazi na kulipa ada kwa wakati | Robo mwaka na Mwaka | Msajili Msaidizi, Msajili, Waratibu wa Madawati, NaCoNGO |
| 5 | Kufanya mikutano ya kisekta ili kutambua mchango, mafanikio na kutatua changamoto za utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Idadi ya mikutano ya Kisekta iliyofanyika Idadi ya taarifa za kisekta zilizowasilishwa | Idadi ya mikutano ya kisekta | Kuhesabu idadi ya mikutano ya kisekta iliyofanyika | Robo mwaka | Msajili Msaidizi, Msajili, Waratibu wa Madawati, NaCoNGO |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Kufanya Jukwaa la Mwaka kwa ajili ya kufanya mapitio ya takwimu, changamoto za utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Kufanyika kwa Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Jumla ya majukwaa ya mwaka yaliyofanyika | Idadi ya Majukwaa ya mwaka yaliyofanyika | Mwaka | Msajili Msaidizi, Msajili, Waratibu wa Madawati |
| 7 | Kufanya mikutano ya majadiliano na jamii ili kuongea na wanufaika wa miradi inayotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Idadi ya mikutano ya majadiliano na jamii iliyofanyika | Jumla ya mikutano ya majadiliano na jamii iliyofanyika | Kuhesabu mikutano ya majadiliano na jamii iliyofanyika na ziara ya ufuatiliaji | Robo mwaka | Msajili Msaidizi, Msajili, Waratibu wa Madawati |
| 8 | Utatuzi wa migogoro ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ndani ya maeneo yao. | Idadi ya migogoro iliyotatuliwa na Wasajili Wasaidizi<br>Idadi ya migogoro iliyohusisha Kamati za Ulinzi na Usalama. Idadi ya migogoro iliyotolewa taarifa | Jumla ya migogoro iliyotatuliwa na Wasajili Wasaidizi na kuhusisha Kamati za Ulinzi na usalama | Kuhesabu Idadi ya migogoro iliyotatuliwa katika taarifa na mahojiano wakati wa ziara za ufuatiliaji | Robo mwaka | Msajili Msaidizi, Msajili, Waratibu wa Madawati, NaCoNGO |

**KIAMBATANISHO 1: VIASHIRIA VYA UTENDAJI KAZI KWA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**

| Na. | LENGO | KIASHIRIA | MAELEZO | NJIA YA UPIMAJI | MUDA | MUHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kuwasilisha taarifa za robo mwaka, mwaka na taarifa za fedha zilizokaguliwa | Idadi ya taarifa zilizowasilishwa | Jumla ya taarifa za robo mwaka, mwaka na taarifa ya fedha zilizowasilishwa | Kukagua nyaraka za taarifa zilizowasilishwa | Robo mwaka<br>Mwaka | Msajili<br>Msajili Msaidizi<br>NGOS<br>Waratibu wa Madawati<br>NaCoNGO |
| 2 | Kutambua wanufaika wa miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyofikiwa kwa mwaka | Idadi ya wanufaika waliofikiwa | Jumla ya wanufaika wa miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali waliofikiwa | Asilimia ya wanufaika katika ripoti za robo na mwaka za Miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Robo mwaka | Msajili<br>Msajili Msaidizi<br>NGOS<br>Waratibu wa Madawati<br>NaCoNGO |
| 3 | Kutambua idadi ya waajiriwa wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Idadi ya waajiriwa | Jumla ya waajiriwa wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali | Kuhesabu waajiriwa katika ripoti na mahojiano wakati wa ziara za kutembelea Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Robo mwaka | Msajili<br>Msajili Msaidizi<br>NGOS<br>Waratibu wa Madawati<br>NaCoNGO |
| 4 | Kutambua utekelezaji wa Mkakati wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Idadi ya miradi ya uendelevu. | Jumla ya vyanzo vya mapato vinavyotumiwa na shirika kuendesha shughuli zake | Kuhesabu vyanzo vya mapato katika Taarifa za fedha za mwaka na Shirika kuwa na Mkakati wa uendelevu | Robo mwaka | Msajili<br>Msajili Msaidizi<br>NGOS<br>Waratibu wa Madawati<br>NaCoNGO |
| 5 | Kutambua kama Shirika linaendeshwa kwa taratibu na sheria | Idadi ya Sera za ndani zilizopo | Jumla ya Sera za ndani zinazotumika katika uendeshaji wa Shirika | Mahojiano wakati wa ziara za kutembelea Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Robo mwaka | Msajili<br>Msajili Msaidizi<br>NGOS<br>Waratibu wa Madawati<br>NaCoNGO |
| 6 | Kutambua miradi iliyotekelezwa na Shirika kwa mwaka | Idadi ya miradi iliyopewa vibali | Jumla ya miradi iliyotekelezwa na shirika kwa mwaka | Kukagua nyaraka za taarifa zilizowasilishwa na ziara za ufuatiliaji | Robo mwaka | Msajili<br>Msajili Msaidizi<br>NGOS<br>Waratibu wa Madawati<br>NaCoNGO |